
# UPENDO MKUU
## And Can It Be That I Should Gain?

Thomas Campbell,1825
Swahili Adoptation by Sir Collins Lwanga
Edited At St Ambrose Parish,Tagaste
DSM, March 2019

Lyricist: Charles Wesley,1738






1.Niwezeje nipate uzima?
Katika Damu ya Mwokozi wangu.
Alinifi-a Pendoni,
Mimi niliyemsulubisha.
Upendo huu wakushangaza kabisa,
wewe Kristu wangu ulinifia Pendoni.

Upendo Mkuu(upendo mkuu),Nashangaa(nashangaa)
Mungu wangu kunifi-a.

2.Kristo wangu alitoa damu.
Siwezi kuelewa Pendo hili.
Viumbe vyo-te vya mbinguni,
navyo haviwezi kufahamu.
Najua tu ni kwa rehema zake Mungu,
Malaika wote wale wamsujudu Mungu.

Ni ve-ma(ni ve-ma), Tumwabudu(tumwabudu)
Tumwamini ndiye mwokozi.

3.Alishuka kutoka mbinguni.
Kwenye ufalme wa Mungu baba yake.
Na utuku-fu aliacha,
afe kwa ajili ya waovu.
Rehema zake ni nyingi na ukarimu,
Kwani Kristo wangu aliniokoa mimi.

Sistahili(sistahili), Neema yake(neema yake)
Lakini aliniokoa.

4.Roho yangu ilifungwa sana.
Dhambi na giza zilinilemea
Ukania-ngaza rohoni,
gereza yangu ikang'aa mno.
Ikafunguka minyororo yangu yote,
Nikaondoka nikaanza kukufuata.

Siku ile(siku ile), Nikapata(nikapata)
Uhuru kweli kwako Mungu.

5.Hukumuni mimi simo sasa.
Mimi ni wake Yesu ndiye wangu.
Yeye ni ki-chwa changu kweli,
na ameniwekea Haki yake.
Kiti hodari sasa kwa kiti cha enzi,
Nimepata taji milele katika Yesu.

Sina hofu(sina hofu), Kusogea(kusogea)
Katika Bwana wangu Kristo.